**KISWAHILI**
**KARATASI 2**
**OCT/NOV. 2005**

**1. SWALI LA KWANZA.**

a)
- Kiingereza ni lugha ya kimataif
- Kiingereza ni lugha rasmi nchini
- Kiingereza ni mojawapo ya lugha zitumiwazo Nairobi
- Ni athari ya waingereza walioitawala nchi hii

(Yoyote 1=alama 2)

b) i)
- Idadi ya watu ni kubwa/watu ni wengi
- Watu huvalia nadhifu/wanawake ni warembo/wanawake huvaa suraali ndefu /wanawake hutengeza nywele zao/wanawake hupaka rangi kucha zao na midomo yao Watu huzungumza Kiswahili na Kiingereza karibu kila wakati. Wanawake wengi hendesha magari yao wenyewe
- Majumba mengine yana maumbo ya kipekee
- Barabara ni nyingi na pana
- Kuna magari mengi ya kila aina
- Wanaume husema Kiswahili na Kiingereza kupitia puani
- Wanaume hutembea kwa maringo wakining'iniza funguo za magari mikononi
- Watoto wa shule husema Kiswahili, Kiingereza na sheng'
- Watu wa Nairobi hutembea Kwa kasi sana bila simile

(zozote 4=1x4 alama 4)

ii)
- Watu huvalia nadhaifu
- Huzungumza Kiswahili na Kiingereza karibu kila wakati
- Wanawake wengi huendesha magari yao
- Wanaume husema Kiswahili na Kiingerexa kupitia puani
- Watu hutembea kwa kasi sana bila simile
- Watoto huzungumza Kiswahili, Kiingereza na sheng'

(zozote 4 =1x4 alama 4)

c) i)
- Ndio kwa sababu watu wa Nairobi ni wengi sana
- La. Anapiga chukukuonyesha wingi wa watu wa Nairobi

(yoyote 1=alama 2)

ii) Ili wapendeze
- Kazi wafanyazo haziwachafui
- Wanajiweza kifedha
- Ili waafiki heshima zao. (yoyote 1=alama 3)

d)
- Limetumika nje ya muktadha/sheng si lahaja (alama 1)

e) i) Fikira/fikra/mawazo/mtazamo (alama 1)

ii) Linalofaa/linalolingana na/linalopatana na/linaloakisi/linalostahiki/linlosadifu (alama 1)

iii) Jumba refu (alama 1)

iv) Waendelee na shughuli/kazi/plikapilka/harakati zao (alama 1)

**SWALI LA PILI**

- Ujambazi wa kimataifa umewasumbua walimwengu sana
- Serikali nyingi zimejitahidi kupambana na janga hili.
- Fanaka haijapatikana.
- Tatizo kubwa ni jelezi la dhana ya ujambazi wa kimataif.
- Watakaburi hawa wanaamini kuwa ujamazi ni wa watu washenzi katika nchi zisizoendelea.
- Kwao ujambazi unaofaa kukabiliwa niwa madawa ya kulevya.
- Unaosababishwa na vinyangarika kutoka ulimwengu wa tatu.
- Vinyangarika hivi ni sharti vifagiliwe ili ustaaragu udumshwe.

b)
- Wamerekani walishtuka na kumaka kuwa taifa lolote au mtu yeyote angethubutu kuwashambulia.
- Hakuna ulimwengu mzima aliyeamini kuwa makrkani ingeweza kushambuliwa
- Huzuni ilitanda ulimwenguni kote.
- Marekani ililipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu huko Afghanistan.
- Wengi duniani walisherehekea
- Tafsiri ya shambulizi hili ilizorota.
- Wengi walidhani kuwa ulikuwa mwanzo wa vita vya wasislamu dhidi ya wakristo.
- Waislamu wote walishukiwa kimakosa kuwa ni majambazi.

**Mtindo wa kutuza**

| | | |
|---|---|---|
| Maudhui | a- | alama 8 |
| | b- | alama 8 |
| Utiririko | - | alama 4 |
| Jumla | | 20 |

**SWALI LA TATU**

a) Yangu- kimilikishi (alama 1)
Maridai- sifa (alama 1)

b) Kulia-Kuliwa (1x2=alama 2)
Kuungia-kuungwa (1x2=alama 2)
(Zozote 4=1x4 alama 4)

c) Jinsi/namna/vile (alama 1)

d) Pahala hap ni pao (alama 1)

e)
1. Kiunganishi
2. Wakati uliopo
3. Mnyambuliko/jinsi ya kufanyana/kufanyiana

(alama 1x3 = alama 3)

f) 1. Majina yanayoanza kwa Ji-katika umoja na MA- katika wingi (alama 1)
Mfano: jina- majina (alama 1)

2. Majina yasiyoanza kwa JI- katika umoja lakini huanza kwa MA- katika wingi (alama 1)
Mfano: somo- masomo (alama 1)

3. Majina yanayoanza kw JI-katika umoja na ME- Katika wing: (alama 1)
Mfano: Jino-meno (alama 1)

4. Majina yanayodumu katika wingi tu, huku yakianza kw MA- (alama 1)
Mfano: maji (alama 1)

g) i) ilinyesha-kitenzi (alama 1)
ii) Mfululizo-kielezi (alama 1)

h) Hatujachukua nguo chanche kuuza (alama 2)

I) i) ndiwe (alama 1)
ii) Ndinyi/ndio. (alama 1)

(j) Safari yangu haikuwa na ugumu wowote ( kwani/ kwa vile/ kwa Sababu/ kwa kuwa/ maadamu) nilikuwa nimejitayarisha vizuri ( alama 2)

(k) (i) Shukurani/ kushukuru/ mshukuriwa
(ii) Mwendo/ kuenda/ mwendewa/ mwendaji; mwendeshaji/ uendeshaji. ( alama 1)

**TANBIHI: MINYAMBULIKO SAHIHI IKUBALIKE**

(l) - Walikuja kutembea kwetu/ walituzuru ( alama 1)
- Walitembea badala / kwa niaba yetu ( alama 1)

(a) (i) - Naona aibu / soni/ haya/ izara/ fedheha/ tayayuri
- Nimetahayari/ nimesusuwaa
(ii) Ni mchoyo/ bahili/ mbafuni; ana mkono gamu/ wa birika ( alama 1)

(b) Kiweto/ koo/ tembe. Mtetea ( alama 1 ½ )
- Mtamba/ mori/ mfarika/ mbarika. Mbuguma/ dachia ( alama 1 ½ )

(c) (i) Zinduna, lulu, ambari ( alama 1 x 3 = alama 3)
(ii) (1) Machapwi; perema
Matumbwitumbwi/ machubwichbwi/ ugonjwa wa kuvimba mashavu ( alama 1)
(2) Tetemaji/ tetekuwanga/ ndui ndogo/ galagala/ homa inayoandamana na vipele mwili wote. ( alama 1)
(iii) buni/ kahawa/ mabuni ( alama 1)